Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo.

Waefeso 2:13

KUFIKA MBINGUNI
NJIA YA KUFIKA MBINGUNI

- **ILI UFIKE MBINGUNI, yakubidi ujue kwamba:**
  "Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." Zaidi ya hayo, bibilia yasema, "Kwa maana mshahara wa hambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu." Warumi 3:23, 6:23

- **ILI UFIKE MBINGUNI, liamini neno la kutia moyo kama Yesu alivyosema:**
  "Nyumbani mwa baba yangu mna makao mengi... nitakuja tena niwakaribishe kwangu, ili nilipo mimi, nanyi muwepo." Yohana 14:2, 3

- **ILI UFIKE MBINGUNI, yakupasa ujue ya kwamba Yesu Kristo:**
  "Alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko" na pia ya kuwa "Ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, ibilisi." Sasa Bwana yu-wasema... "Mimi ndimi niishiye nami nalikuwa nimekufa, na tazama. ni hai hata mileje, Amina, Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu." 1 Wakorintho 15:3, Waebrania 2:14, Ufunuo wa Yohana 1:18

- **ILI UFIKE MBINGUNI, sharti ujue ya kwamba wokovu ni karama ya Mungu isiyo na malipo, kwa sababu wenye dhambi wakitubu:**
  "Huokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu." Yesu Kristo anena hivi "Mimi ndimi mlango, mtu akiingia kwa mimi, ataokoka."
  Waefeso 2:8, Yohana 10:9

Matumaini
kwa wasio na matumaini

MUNGU AMEKUANDALIA NJIA YA KWENDA MBINGUNI

MUNGU AKUSHAURI JINSI UNAVYO WEZA KUMSHINDA SHETANI:

“Nao wakamshinda,	Hakikisho hili lamaanisha kwamba umewezeshwa kumshinda ibilisi kabisa. Yeye shetani, adui wa Mungu, hukushtaki wewe jinsi ulivyo mwenye dhambi na makosa mengi. Shetani anapenda sana ujifikirie kuwa huna tumaini la kuingia mbinguni.
kwa damu ya Mwana Kondoo,	Hivyo ni kumaanisha ya kwamba wanadamu wanayo mbegu ya kifo katika damu yao. Lakini ni damu yake Bwana Yesu tu iliyo safi, na yenye uzima. Na ni damu hiyo yake iliyomwagika ili usamehewe dhambi zako ukimwamini Bwana Yesu Kristo. Baada ya kuokolewa naye, shetani hataweza kukushtaki tena: Utakuwa tayari umekombolewa na damu yake Yesu Kristo. Hutakuwa gerezani mwa shetani.
na kwa neno la ushuhuda wao,	Itakubidi umshuhudie mwingine kwamba umekata shauri kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wa maisha yako.
ambao hawakuyapenda maisha yao hata kufa *- Ufunuo 12:11*	Hivi ni kumaanisha ya kwamba kwa sababu Bwana na Mwokozi Yesu alikufa kwa ajili yako, sasa mapenzi yako kwake yamezidi kipimo cha jinsi ujipendavyo na pia jinsi unavyoyapenda maisha haya. Huku ukiyatumia maneno yako mwenyewe, mwambie jinsi unavyompenda Yesu kadiri masivu.

Kwa uwezo wa damu yake Bwana Yesu ya dhamana namuacha shetani kabisa, namkataa kata kata.

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”
Yohana 3:16

Yakulazimu uombe kwa dhati na ukweli, huku ukijinyenyekeza kabisa, na kutubu; ili uupokee upendo wake Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo njia pekee ya kuurithi uzima wa milele. Vile utakavyoishi milele yategemea ombi lako liifuatayo rehema na neema yake Mungu wetu. Ukiomba kwa roho na nia hiyo, utaupokea upendo wa kutoka kwake baba Mungu. Sasa omba kama ifuatavyo:

OMBI LANGU

Ewe Mungu wa Uwezo wote, nimepiga magoti mbele yako. Nakiri ya kwamba ni mwenye dhambi. Ninastahili kufa kwa ajili ya dhambi zangu. Nakushukuru kwa kumtuma Yesu asulubiwe msalabani pahali pangu mimi. Sasa naziacha dhambi zangu hapa na kumwamini Yesu Kristo awe bwana na Mwokozi wangu. Naomba sasa unisamehe,unitakase ili niishi jinsi upendavyo. Kwa uwezo wa damu yake Bwana Yesu ya dhamana namuacha shetani kabisa, namkataa kata kata. Sasa mimi nakualika ewe Bwana Yesu uje ndani ya moyo wangu na maisha yangu. Nijaze na Roho Mtakatifu. Asante Yesu kwa kunisamehe. Asante kwa kunizaa upya. sasa ninalo hakikisho la kuishi nawe mbinguni. Amina!

Trans World Radio • P.O. Box 21514 (00505), Nairobi, Kenya Call us at - 387 3938 /20 /46
©CCIM